(a) *Mwenyekiti*.—Mwenyekiti atasimamia mikutano yote ya komiti za tawi pamoja na Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka. Atakuwa msemaji wa tawi katika shughuli zote zinazohusu Chama.

(b) *Naibu wa Mwenyekiti*.—Naibu wa Mwenyekiti atafanya kazi kama inavyoonyeshwa (a) juu wakati mwenyekiti mwenyewe hayupo.

(c) *Naibu*.—Katibu ataweka rekodi pamoja na kumbukumbu za shufulu zote, zikiwa ni pamoja na mikutano ya Chama. Atatoa noti za kufanywa kwa mikutano ya Chama na kufanya kazi zote kama atakavyoagizwa mara kwa mara na komiti, ikiwa ni pamoja na kushughulikia mawasiliano ya barua.

(d) *Naibu wa Katibu*.—Naibu wa Katibu atachukua wadhifa wa katibu wakati mwenyewe hayupo na kufanya kazi nyinginezo zitakazoagiziwa kwake mara kwa mara na Komiti Kuu ya Tawi ama Katibu.

(e) *Mweka Hazina*.—Mweka Hazina atatunza pesa zote za Chama pamoja na uhasibu; atatarisha na kutoa kwa komiti ripoti kuhusu hesabu ya pesa na matumizi yake.

(f) *Naibu wa Mweka Hazina*.—Naibu wa Mweka Hazina atafanya kazi za Mweka Hazina wakati mwenyewe hayupo; na atashughulikia mashauri yote kama atakavyoagizwa kufanya na Mweka Hazina ama komiti.

(g) *Katibu Mtendaji*.—Katibu Mtendaji atatarisha na kusimamia mipango ya shughuli za Chama na kuhakikisha kwamba idara zote za Chama zinatekeleza wajibu wake vilivyo, zikiwa ni pamoja na Vijana na Makundi ya Akina Mama.

(h) *Afisa Mkuu wa Tawi*.—Atakuwa kama Afisa wa Mapato wa Chama katika wilaya. Atasimamia na kuendeleza shughuli za Chama, na hasa wakusanyaji wa ada katika wilaya. Pesa zote

zinazostahili kulipwa kwa Chama ama zinazodaiwa na Chama zitalipwa kwake. Atapeleka pesa kama hizo kwa Mweka Hazina wa Kitaifa na Mweka Hazina wa Tawi kulingana na kiwango cha asilimia kilichowekwa kuambatana na Kifungu 21 (c) cha Katiba. Afisa Mkuu wa Tawi la Wilaya atasaidia katika utayarishaji wa taarifa ya matumizi ya pesa itakayotumwa kwa Mweka Hazina wa Kitaifa kila mwezi.

9. TAWI NDOGO (SEHEMU YA UCHAGUZI)

Kila tawi, kwa manufaa ya maongozi thabiti, litagawanywa katika matawi madogo madogo yatakayosimamiwa kuambatana na sehemu za Uchaguzi za Bunge la Taifa kote nchini.

(a) Tawi litasimamiwa na Komiti Maalum itakayokuwa na:

- (i) Mwenyekiti, Naibu wa Mwenyekiti, Katibu, Naibu wa Katibu, Mweka Hazina na Naibu wa Mweka Hazina.
- (ii) Kiongozi wa Vijana katika Tawi, Kiongozi wa Kina Mama pamoja na Makatibu wa Wanayusi na Kundi la Kina Mama.
- (iii) Kiongozi, atakayeteuliwa na Komiti Kuu ya Tawi iki-saidiana na Komiti ya Shughuli Maalum ya Tawi, ambaye atasimamia kazi ya wakusanyaji pesa katika tawi na kusaidia katika shughuli za usimamizi chamani.
- (iv) Mwenyekiti na Katibu kutoka katika kila Komiti Maalum ya Lokesheni/Wodi.
- (v) Mbunge wa sehemu hiyo.

(b) Kazi ya komiti za matawi madogo itakuwa:

- (i) Sawa na jinsi ilivyo katika matawi makubwa, ila matawi hayo hayatakuwa na uwezo wa kumsimamisha mwanachama ye yote, badala yake yatatoa ripoti kuhusu ukosefu wa nidhamu wa mwanachama anayehusika kwa Mwenyekiti wa Tawi ambaye atatoa ripoti yake mbele ya Komiti Kuu ya Tawi.

(ii) Pesa zote zitakazokusanywa zitalipwa na wakusanyaji wa kila lokesheni moja kwa moja kwa Afisa Mkuu wa Tawi na tawi ndogo litapeleka maombi yake ya kutaka msaada kwa Komiti Kuu, kupitia kwa Mweka Hazina wa Tawi.

(c) (i) Komiti itafanya mkutano wa kila mwaka kabla ya Juni 30.

(ii) Mkutano huo utahudhuriwa na:

(a) Maafisa wa Tawi.

(b) Wajumbe ishirini kutoka katika kila lokesheni/wodi katika tawi hilo. mradi idadi hiyo iwe na waakilishi watano wa Vijana na watano wa Kina Mama.

(iii) Mikutano hiyo itazungumzia yafuatayo katika ajenda:

1. Kuidhinisha maswala yaliyozungumziwa kwenye mkutano uliopita pamoja na yale yaliyotokana na maswala hayo.
2. Taarifa ya Katibu.
3. Taarifa ya Mweka Hazina kuhusu pesa zilizotumika iliyokaguliwa na Afisa Mkuu.
4. Hotuba ya Mwenyekiti.
5. Shughuli nyinginezo kufuatia idhini ya Mwenyekiti.

10. KOMITI YA LOKESHENI/WODI

(a) Kila tawi ndogo litagawanywa kwa lokesheni/wodi. Kila lokesheni/wodi itasimamiwa na Komiti ya Lokesheni/Wodi itakayokuwa na:

(i) Mwenyekiti, Naibu wa Mwenyekiti, Katibu, Naibu wa Katibu, Mweka Hazina, Naibu wa Mweka Hazina ambao watakuwa maafisa wa tawi.

(ii) Kiongozi wa Vijana na Kiongozi wa Kundili la Kina Mama.

(iii) (a) Katika Lokesheni: Mwenyekiti na Katibu kutoka kila lokesheni ndogo.

(b) Katika Wodi: Wanachama kumi watakaochaguliwa kila baada ya miaka mitano katika Mkutano wa kila Mwaka wa Wanachama wote wa KANU katika wodi.

(iv) Diwani anayewakilisha wodi/lokesheni inayohusika.

(b) Kazi ya Komiti Maalum ya Lokesheni/Wodi itakuwa sawa na ya tawi, lakini katika kiwango cha lokesheni. Ukusanyaji wa pesa na ada za uanachama ni lazima kusimamiwa na kupelekwa kwa Afisa Mkuu wa Tawi. Komiti za lokesheni/wodi zitatuma maombi ya kutaka pesa kwa Mweka Hazina wa Tawi kupitia kwa matawi madogo ili yaweza kufikiriwa na Komiti Kuu ya Tawi.

(c) Lokesheni/wodi itakuwa na mkutano wa kila mwaka kabla ya Mei 31 kila mwaka. Katika wodi, mkutano huo utahudhuriwa na wanachama wote wa KANU waliolipa ada zao kikamilifu katika sehemu inayohusika. Yatakozongumziwa katika ajenda kwenye kila Mkutano wa Mwaka ni pamoja na:

(i) Maswala yaliyojadiliwa kwenye mkutano wa mwisho wa lokesheni/wodi pamoja na yale yaliyotokana na maswala hayo.

(ii) Ripoti ya Katibu.

(iii) Tarifa ya Mweka Hazina kuhusu jinsi pesa zilivyotumiwa pamoja na taarifa ya pesa zilizotumwa katika Makao Makuu ya Wilaya na kukaguliwa na Afisa Mkuu wa Wilaya.

(iv) Hotuba ya Mwenyekiti.

(v) Shughuli nyinginezo.

(d) Wakusanyaji pesa katika lokesheni/wodi watateuliwa na Komiti Kuu ya Tawi. Kila mkusanyaji atapatiwa Beji Maalum yenye nambari na ambayo itatumiwa wakati wote anapokuwa kazini.

11. KOMITI YA LOKESHENI NDOGO

Kila lokesheni itagawanywa katika lokesheni ndogo ndogo kulingana na utaratibu wa utawala wa lokesheni hizo. Kila lokesheni ndogo itasimamiwa na Komiti ya Lokesheni Ndogo, itakayokuwa na wafuatao:

- (i) Mwenyekiti, Naibu wa Mwenyekiti, Katibu, Naibu wa Katibu, Mweka Hazina, na Naibu wa Mweka Hazina ambao watakuwa maafisa wa Chama.
- (ii) Kiongozi wa Kina Mama na Kiongozi wa Wanayusi.
- (iii) Wanachama kumi waliochaguliwa kila baada ya miaka mitano kwenye Mkutano wa Kila Mwaka.

12. UCHAGUZI WA MAAFISA WA KANU

Uchaguzi utafanywa kila baada ya miaka mitano.

- (i) Kwenye mkutano wa lokesheni ndogo/wodi wanachama wote waliolipa ada zao za KANU watahudhuria na kushiriki kwenye shughuli zote za uchaguzi.
- (ii) Katika lokesheni, mkutano wa KANU kwenye kila wodi utakuwa na waakilishi 20, watano wakiwakilisha Kundi la Kina Mama na wengine 5 wakiwa ni waakilishi wa Vijana na watakuwa ni pamoja na maafisa wa lokesheni ndogo.
- (iii) Katika mkutano wa tawi, kila komiti ya lokesheni/wodi itawakilishwa na wajumbe 20 watano wakiwa ni kina mama na watano wanayusi wakiwa ni pamoja na maafisa wa lokesheni/wodi.

- (iv) Maafisa wote wa tawi la Chama watachaguliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Chama kwa kufuata utaratibu wa kusimama nyuma ya mgombea uchaguzi. Watatumika kwa kipindi cha miaka mitano na wanaweza kujitokeza kugombea uchaguzi tena baada ya kumalizika kwa kipindi hicho. Kwenye mkutano wa tawi, kila tawi ndogo litawakilishwa na wajumbe 100 ambao watateuliwa kisawa kutoka katika kila lokesheni/wodi katika tawi linalohusika.
- (v) Maafisa wa Kitaifa—Maafisa wote wa kitaifa wa Chama watachaguliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Wajumbe kwa kura ya kisiri. Watatumika kwa kipindi cha miaka mitano na wataweza kujitokeza kugombea uchaguzi tena baada ya kumalizika kwa kipindi hicho.

13. KUNDI LA WABUNGE WA KANU

(a) Wanachama wote katika Bunge la Taifa watakuwa kwenye Kundi la Wabunge wa KANU.

(b) Kundi la Wabunge wa KANU litakuwa chini ya usimamizi wa Rais wa Chama ambaye atawasiliana na Komiti Kuu ya Kitaifa na Baraza Kuu la Kitaifa kuhusu shughuli na mienendo ya Kundi la Wabunge wa KANU.

(c) Kundi la Wabunge wa KANU litawajibika kushughulikia utaratibu na mipango katika Bunge, lakini halitakuwa na uwezo wa kuanzisha mwongozo mpya. Litawasiliana mara kwa mara na Baraza Kuu la Kitaifa

(d) Wote katika kundi hili, wakiwemo Mawaziri wanaweza kuhitajiwa kulipa ushuru muda baada ya muda na Kamati Kuu ya Chama.

14. KUNDI LA VIJANA WA KANU

(a) Watakaokubaliwa kujiunga na kundi hili watakuwa wanachama wa KANU ambao wametimiza umri wa miaka 18 lakini bado hawajafikisha umri wa miaka 35. Maombi ya kutaka kujiunga na kundi hili yatafanywa moja kwa moja kwa maneno ya mdomo au katika maandishi kwa Katibu wa Chama cha

KANU katika lokesheni ndogo au wodi inayohusika. Mwanachama akisha kubaliwa kundini, atapewa kadi au kitambulisho maalum cha Kundi la Vijana wa KANU.

(b) Kila mwanachama wa Kundi la Vijana wa KANU atalipa ada ya Sh. 10 kwa mwaka.

(c) Ingawa vijana hawa wa KANU watapewa uwezò fulani wa kujiamulia mambo fulani na kujitambulisha kama kikundi, kundi hili la vijana wa KANU litakuwa daima sehemu moja ya Chama na kubaki chini ya usimamizi wake na kunidhamishwa katika lokesheni ndogo, lokesheni au wodi na hali kadhalika katika tawi.

(d) KAMATI YA KUNDI LA VIJANA WA KANU KATIKA
LOKESHENI NDOGO/WODI

Kila Kamati ya Kundi la Vijana wa KANU katika lokesheni ndogo itakuwa ni pamoja na wafuatao:

(i) Mwenyekiti, Katibu na Katibu Mtendaji.

(ii) Wanachama kumi.

(e) KAMATI YA KUNDI LA VIJANA WA KANU KATIKA
LOKESHENI

Kamati ya Kundi la Vijana wa Kanu katika lokesheni itakuwa ni pamoja na:

(i) Mwenyekiti, Katibu na Katibu Mtendaji.

(ii) Mwenyekiti na Katibu kutoka Kundi la Vijana wa KANU katika kila lokesheni ndogo.

(f) KAMATI YA KUNDI LA VIJANA WA KANU KATIKA TAWI
NDOGO

Kamati ya Kundi la Vijana wa Kanu katika Tawi Ndogo la Chama itakuwa ni pamoja na wafuatao:

(i) Mwenyekiti, Katibu na Katibu Mtendaji.

(ii) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Kundi la Vijana wa Kanu wa Lokesheni/Wodi.

(g) KAMATI YA KUNDI LA VIJANA WA KANU KATIKA TAWI

Kamati ya Kundi la Vijana wa KANU katika tawi itakuwa kama ifuatavyo:

(i) Kiongozi wa vijana wa KANU katika tawi, katibu na Katibu Mtendaji.

(ii) Mwenyekiti na Katibu kutoka kila kamati katika Tawi ndogo.

(h) MKUTANO MKUU WA MAKUNDI YA VIJANA

(i) Makundi ya vijana yatafanya mikutano yao mikuu wakati mmoja na ile ya kamati zingine za Chama zinazohusiana kikatiba.

(ii) Uchaguzi wa maafisa wa makundi yao mbali mbali utafanywa katika mikutano hiyo mikuu.

(iii) Kwenye Mkutano Mkuu wa Kundi la Vijana katika lokesheni ndogo/wodi, wanachama wote wa Kundi la Vijana wa KANU ambao wamelipa kwa ukamilifu ada zao watakuwa huru kushiriki katika mambo yote kwenye mkutano huo pamoja na uchaguzi.

(iv) Kwenye mkutano mkuu wa vijana katika lokesheni, kila lokesheni ndogo itawakilishwa na wajumbe watano na maafisa wote wa Kundi la Vijana katika lokesheni hiyo.

(v) Kwenye mkutano mkuu wa vijana wa KANU katika tawi ndogo, kila lokesheni itawakilishwa na wajumbe watano na maafisa wote wa tawi hilo ndogo.

(iv) Mkutano mkuu wa vijana wa KANU katika tawi utahudhuriwa na wafuatao:

(a) Maafisa wote wa Kundi la Vijana katika tawi hilo.

- (b) Wanakamati wa Kundi la Vijana katika tawi.
 - (c) Wajumbe 10 kutoka kila kamati ya kundi la vijana katika tawi ndogo.
 - (d) Afisa Mkuu wa Chama katika tawi.
- (i) Kwenye mkutano mkuu wake wa kila mwaka Kundi la Vijana katika tawi litakuwa na yafuatayo katika ajenda:
 - (i) Mdondoo ya mkuu wa kila mwaka uliotangulia wa kundi na mambo mengineyo ambayo yataweza kuzuka kutokana na madondoo hayo.
 - (ii) Taarifa ya Katibu wa vijana katika tawi.
 - (iii) Ratiba ya miradi ya kujisaïdia wenyewe.
 - (iv) Mambo mengineyo ya kujadiliwa, kwa ruhusa kutoka kwa kiongozi.
 - (j) Shughuli kamili za kundi hili zitakuwa kama ifuatavyo:
 - (i) Kutimiza kazi zao kwa ushirikiano na kamati za Chama katika tawi, tawi dogo, lokesheni na wodi ili kuhakikisha kwamba mipango na maongozi ya Chama yanafanikishwa.
 - (ii) Vijana hawa hawatakuwa na ruhusa ya kuchuma mali na kuyatumia wapendavyo kwa niaba ya Chama, lakini matawi ya Chama yatakuwa yakiwapa kiasi fulani cha pesa ili kuwawezesha kutimiza wajibu wao.
 - (iii) Wataweza kutayarisha na kuendesha miradi ya kujisaidia wenyewe, kufanya kazi za kujitolea, kutayarisha mikutano ya vijana, michgozo na mikutano miongoni mwa vijana katika wilaya.
 - (k) Rais wa Chama anaweza kuitisha Mkutano wa Kitaifa wa Vijana muda baada ya muda na kuusimamia mwenyewe.

- (i) Mkutano kama huo utahudhuriwa na wawakilishi sita kutoka kila tawi ambao watachaguliwa na kamati ya Kundi la Vijana wa KANU katika tawi.
- (ii) Mkutano huo utajadili mambo kadha wa kadha kama yatakavyopangwa na Rais.

15. KUNDI LA KINA MAMA WA KANU

(a) Uanachama wa Kundi la Kina Mama wa KANU uko wazi kwa kina mama wote waliolipa ada kamili kama wanachama wa KANU.

(b) Muundo na mpangilio wa Kundi la Kina Mama wa KANU utakuwa sawa kwa kila njia na ule wa Makundi ya Vijana wa KANU kama inavyoelezwa katika kifungu 14, (a), (b), (c), (d), (e), (f), (g), (h), (i), (j), na (k).

(c) Kundi la Kina Mama litakuwa na viongozi katika tawi ambao watafanya kazi bega kwa bega na maafisa wa Ustawi wa Jamii ili kusaidia katika uanzishaji wa miradi ya kujisaidia wenyewe na vile vile makundi ya kujitolea. Makundi ya Kina Mama wa KANU yataweza kujitayarishia semina, vikundi vya kubadilishana mawazo, vikundi vya kisomo cha watu wazima, mikutano ya hadhara ya kina mama na shughuli nyinginezo zenye nia ya kukuza mawazo ya kina mama nchini kuhusu mambo mbali mbali ya kitaifa.

16. UHUSIANO WA KIMATAIFA

(a) Idara inayohusika na uhusiano wa kimataifa itachunguza kwa makini mashauri yote yanayohusiana na Chama uwakilishi katika mataifa ya kigeni, kuhudhuria mikutano na upokeaji wageni na kuwaongoza hadi mbele ya Rais na Kamati Kuu ya Chama.

(b) Hakuna mwanachama au afisa ye yote wa Chama ambaye anaweza kuzuru taifa la kigeni, kukubali misaada ya masomo, pesa au aina yo yote ile ya usaidizi ijapokuwa iwe kwamba kitendo kama hicho kilikuwa kimeidhinishwa awali na Kamati Kuu ya Kitaifa ya Chama cha KANU na hali kadhalika kibali kwenye maandishi kilichotolewa na Rais.

17. IDADI YA KUTOSHA KWA MKUTANO KUWAHI KUFANYWA

(a) Idadi ya kutosha kwa Mkutano wa Kamati Kuu ya Kitaifa na Baraza Kuu la Kitaifa la Chama cha KANU itakuwa nusu ya wanachama wake.

(b) Idadi ya kutosha kwa Mikutano ya Wajumbe, na mikutano yote mikuu katika tawi, tawi ndogo na lokesheni/wodi itakuwa theluthi mbili ya watu wenye haki ya kuhudhuria mikutano kama hiyo.

(c) Idadi ya kutosha kwa mikutano ya kamati kuu ya tawi, tawi ndogo, kamati ya utekelezaji katika lokesheni/wodi na kamati zote za makundi ya kina mama na vijana itakuwa nusu ya idadi kamili inayostahili kuhudhuria mikutano kama hiyo.

(d) Idadi ya kutosha kwa Mkutano wa Kundi la Wabunge wa KANU itakuwa theluthi mbili ya wanachama wake.

18. MAGAZETI NA UCHAPISHAJI

(a) Chama kinaweza kuwa na magazeti yake na kuendesha mitambo ya uchapishaji au kununua hisa katika mitambo iliyoko ya uchapishaji.

(b) Chama kinaweza kuchapisha magazini yake, vitabu, vijitabu, makaratasi mengine ya mara kwa mara, na kadhalika.

(c) Kutakuwepo na Kamati ya Habari na Uhusiano Mwema itakayoteuliwa na Kamati Kuu ya Chama.

19. MAHIHISHO YA KATIBA NA KANUNI ZA CHAMA

Katiba na kanuni za Chama zinaweza kusahihishwa kwa azimio litakalopitishwa kwa wingi wa kura na theluthi mbili za idadi ya wanachama wanaohudhuria mkutano wo wote wa wajumbe wa Chama. Ni matawi ya Chama pekee na Kamati Kuu ya Kitaifa ya Chama inayoweza kudhamini maazimio ya kutaka kusahihisha katiba na kanuni za Chama na kuyatuma kwa Mkutano wa Wajumbe ili yafikiriwe.

20. UTARATIBU WA MIKUTANO

(a) Mikutano yote ya Kamati Kuu ya Kitaifa, Baraza Kuu la Kitaifa, Kundi la Wabunge wa KANU au Mkutano wa Wajumbe, itafanywa chini ya uenyekiti wa Rais au ikiwa hayupo, chini ya Makamu wa Rais au ikiwa Rais na Makamu wa Rais hawapo, chini ya Mwenyekiti wa Taifa wa Chama. Mikutano katika tawi, tawi ndogo, lokesheni au wodi itaongozwa na Mwenyekiti au ikiwa Mwenyekiti hayupo na Mwenyekiti Mdogo.

Ikiwa maafisa hawa wawili hawapo, mikutano hii inaweza kuongozwa na mwanakamati ye yote ambaye atachaguliwa kwenye mkutano huo.

(b) Mwenyekiti, akipenda, anaweza kupunguza idadi ya watu walioruhusiwa kuzungumza na kuunga mkono au kupinga mswada, isipokuwa mswada wa kupinga kufungwa kwa majadala upitishwe kwa wingi wa kura na theluthi tatu ya waliohudhuria mkutano huo.

(c) Isipokuwa iwe imeelezwa vingine katika katiba hii, maazimio yataamuriwa na kupitishwa kwa wingi wa kura kwa kufuata utaratibu wa upigaji kura wa kawaida. Kura zitapigwa kwa kuinua mikono juu.

(d) Ikiwa kwenye upigaji kura katika mkutano wo wote, idadi ya wanaopinga itakuwa sawa na ile ya wanaouunga mkono, basi Mwenyekiti ataruhusiwa kupiga kura yake.

21. FEDHA

(a) Kila mwanachama wa Chama cha KANU atalipa ada yake ya uanachama au malipo yake ya kila mwaka kwa kundi lake katika lokesheni yake ndogo au wodi kwa sababu ni hapa katika lokesheni ndogo au wodi ambapo mwanachama atajiandikisha.

(b) Kila kundi la KANU katika kila lokesheni ndogo litapeleka pesa zote zilizokusanywa kutokana na ada ya uanachama na mapato yo yote ya kila mwezi, kwa Makao Makuu ya Chama katika tawi. Kanuni hii ndiyo itakayofuatwa katika matawi ndogo/wodi kila mara ada au malipo hayo yanapokelewa.

(c) Fedha za Chama zitagawanywa kama inavyofuata:

- (i) Nusu ya jumla ya pesa zinazopokelewa na makao makuu ya tawi kutoka lokesheni ndogo/wodi kama ada ya uanachama na malipo ya kila mwezi, itabaki kwenye tawi hilo na nusu kutumwa katika Makao Makuu ya Kitaifa ya Chama.
- (ii) Matawi yatahakikisha kwamba zaidi ya asilimia 20 ya pesa zilizopokelewa kutoka lokesheni ndogo zinarudishwa huko ili kulipia gharama zo zote katika tawi ndogo, lokesheni na lokesheni ndogo/wodi.
- (iii) Ada ya uteuzi itagawanywa ifuatavyo:

Uchaguzi wa Bunge: nusu itabaki katika tawi na nusu kutumwa katika makao makuu ya KANU. Uchaguzi wa madiwani: nusu itatumwa kwa tawi na nusu kupelekwa katika Makao Makuu ya Chama.

Waweka Hazina wote wa matawi yote ya Chama watatoa taarifa ya fedha kwa Mweka Hazina wa Kitaifa kila mwezi. Taarifa hiyo ipokelewe kabla au katika juma la kwanza la mwezi na ieleze kwa kinaganaga jumla ya pesa zilizopokelewa kutoka lokesheni ndogo/wodi zote katika wilaya na kiasi kilichotumwa katika Makao Makuu ya Chama.

(d) Pesa zote zitakazokusanywa kwenye mikutano ya harambee zitabaki katika kundi lililotayarisha harambee hiyo na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa kabla ya harambee kama hizo kutayarishwa.

(e) Pesa zote zitakazopokelewa na Mweka Hazina wa Kitaifa, Mweka Hazina wa Tawi, Mweka Hazina wa Tawi Ndogo/Wodi zitahifadhiwa kwenye akaunti katika banki au Akiba ya Posta iliyoidhimishwa na Kamati Kuu ya Kitaifa ya Chama/Kamati Kuu ya Chama katika Tawi.

(f) Hakuna pesa zo zote zitakazotolewa kwenye akaunti ya banki au Posta kwa malipo yo yote bila azimio kupitishwa kwanza na Kamati Kuu ya Kitaifa au Kamati Kuu ya Tawi inayohusika na

utunzaji wa akaunti hiyo. Hundi au fomu zo zote za kutoa pesa kwenye akaunti hiyo zitatiwa sahihi na maafisa watatu wa kamati, mmoja wao akiwa ni Mweka Hazina, au mtu mwingine ye yote aliyepewa kibali cha kutia sahihi kama Mweka Hazina hayupo.

(g) Makundi ya kina mama na vijana wa KANU yatafuata utaratibu huu kuhusu upokeaji matumizi ya fedha na Mweka Hazina daima ataweka tafadhali ya pesa zote zilizotumiwa. Tafadhali kama hiyo itachunguzwa daima na Afisa Mkuu wa Chama katika Tawi. Pesa zote zitakazokusanywa na makundi haya mawili zitatolewa kwa Mweka Hazina wa Tawi. Kamati Kuu ya Tawi itaidhinisha bajeti na gharama ya makundi hayo.

(h) Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Chama daima atakuwa na uwezo wa kuchunguza na kukagua hesabu za fedha za Chama na pia maazimio yaliyopitishwa kuidhinisha matumizi ya fedha za Chama. Mkaguzi/Mhasibu wa Chama atachunguza taarifa ya hesabu ya fedha ya kila mwaka iliyotayarishwa na Mweka Hazina wa Kitaifa kabla ya kutolewa mbele ya Mkutano wa Kila Mwaka wa Wajumbe na kuidhinisha ikiwa ni ya kweli au la.

(i) Nakala ya ripoti ya mkaguzi kuhusu hesabu ya fedha na taarifa ya hesabu ya fedha iliyotayarishwa na Mweka Hazina wa Kitaifa itatumwa kwa kila tawi la Chama na kwa kila mwanakomiti wa Kamati Kuu ya Kitaifa, wakati mmoja na arifa ya kuitisha mkutano mkuu wa kila mwaka wa wajumbe wa Chama.

(j) Kila tawi, katika mkutano wake wa kila mwaka, litamteua mkaguzi wa hesabu ya fedha aliyehitimu.

(k) Mkaguzi wa Fedha za Tawi atakuwa na uwezo daima wa kukagua hesabu zo zote za fedha za tawi na pia taarifa ya kila mwaka ya hesabu ya fedha iliyotarishwa na Mweka Hazina wa Tawi. Nakala ya hesabu hizo zilizokaguliwa, itatumwa kwa tawi ndogo na nakili tatu kupelekewa Makao Makuu ya Chama.

(l) Kamati Kuu ya Kitaifa itateua mkaguzi wa vitabu ambaye atakagua au kuamuru hesabu ya pesa katika matawi kukaguliwa. Mkaguzi huyo wa vitabu, au mtu ambaye amepewa kibali naye katika maandishi, atapewa haki ya kuvikagua vitabu vya hesabu ya pesa vya Chama katika kila mahali.

(m) Kamati Kuu ya Kitaifa itakuwa na uwezo wa kumsimamisha chamani mwanachama ye yote au afisa ye yote wa Chama ambaye:

(i) Atapatikana na kosa la matumizi mabaya ya pesa za Chama.

(ii) Itagunduliwa anayapuuza maagizo na kanuni katika katiba hii mara kwa mara, au kanuni zinginezo zitakazowekwa na Baraza Kuu la Kitaifa kwa manufaa ya usimamizi bora wa fedha za Chama katika Makao Makuu, katika tawi, tawi ndogo na lokesheni ndogo/wodi.

(n) Pesa za Chama zitatumika katika kuendeleza mbele malengo na makusudio ya Chama.

(o) Chama kitakuwa huru kupokea misaada ya pesa au usaidizi wa aina yo yote halali.

(p) Kamati Kuu ya Kitaifa itahakikisha kwamba taarifa ya hesabu ya fedha za Chama inatayarishwa kila baada ya miezi mitatu na kukabidhiwa Baraza Kuu la Kitaifa.

(q) Mweka Hazina anaweza kuruhusiwa kukaa na kiasi fulani cha pesa kitakachoidhinishwa na Kamati Kuu ya Kitaifa, Kamati Kuu ya Tawi na Kamati ya Utekelezaji katika Tawi Ndogo, kwa matumizi ya dharura. Hesabu kamili kuhusu matumizi hayo ni sharti iwekwe na kutunzwa na Mweka Hazina anayehusika ambaye ataweza kuzitumia fedha hizo baada ya kujaza fomu ya kuonyesha kazi ya pesa hizo na kushuhudiwa na watu wengine wawili mbali na Mweka Hazina.

22. UTARATIBU UTAKAOFUATWA WAKATI WA UTEUZI WA WAGOMBEA UCHAGUZI KWA KUTUMIA TIKITI YA CHAMA

(a) Wagombea uchaguzi katika Serikali za Wilaya:

(1) Mwanachama ye yote wa Chama cha Kenya African National Union mwenye nia ya kugombea kiti cha udiwani katika Serikali za Wilaya ni sharti atume

maombi kwenye fomu maalum ya KANU ya maombi kama hayo kwa kamati kuu ya Chama cha Kenya African National Union katika tawi yakiwa yana-ambatanishwa na historia fupi kuhusu mwenye maombi hayo. Nakala ya maombi hayo itumwe kwa Katibu Mkuu wa Chama na iwe ni pamoja na yafuatayo:

- (i) Jina kamili la mwenye maombi.
 - (ii) Nambari yake iliyoandikishwa ya kupiga kura.
 - (iii) Namba yake ya uanachama.
 - (iv) Jina la tawi lake ndogo.
- (b) Na hali kadhalika mwenye nia ya kugombea uchaguzi:
- (i) Sharti awe na hati halisi ya uanachama wa maisha wa Chama cha KANU.
 - (ii) Sharti awe hajatenda kosa lo lote la kihalifu maishani mwake au kujishughulisha wala kuhusika na vitendo vya uchochezi na ufisadi.
 - (iii) Ni sharti atimize masharti yote ya uchaguzi kulingana na katiba ya Kenya.
- (2) Afisa Mkuu wa Chama katika tawi atatoa fomu za KANU za maombi ya kugombea uchaguzi kwa mwenye nia ya kugombea uchaguzi na hali kadhalika fomu za kukariria kiapo cha uaminifu. Kila mwenye maombi ni sharti atume nakala moja ya fomu ya maombi iliyojazwa kwa ukamilifu kwa Mwenyekiti wa Tawi kulingana na Kanuni Namba 1, na nyingine kwa Katibu Mkuu.
- (3) Maombi hayo yataandamana na ada ya shilingi elfu moja mia tano (Sh. 1,500) ambazo hazitaweza kurudishiwa mwenyewe.
- (4) Kamati Kuu katika Wilaya zitawahoji wote wanaotaka kugombea viti katika Serikali za Wilaya na kutoa taarifa yao kwa Makao Makuu ya Chama:

- (5) Kila mgombea uchaguzi kwa tikiti ya Chama cha Kenya African National Union anayewania kiti cha udiwani sharti atie sahihi fomu ifuatayo ya ukariri wa kiapo cha uaminifu. Fomu hii baada ya kutiwa sahihi na mwenye maombi, itaambatanishwa na dhamana kama ilivyotajwa katika aya ya tatu katika kanuni hii.

KIAPO CHA UAMINIFU

Mimi
ninayetaka kusimama kama mgombea kiti wa KANU katika uchaguzi ujao wa Serikali za Wilaya naapa ya kwamba:

- (i) Nitakuwa mwaminifu kwa Rais wa Chama wakati wote.
- (ii) Nitaunga mkono daima katiba ya Chama na misingi yake yote ya kukuza umoja miongoni mwa Wakenya.
- (iii) Nitaunga mkono daima, tena kwa dhati mwongozo wa KANU na maongozi ya mipango yake ya Ustawi na pia Serikali yake, na
- (iv) Nitafuata daima katiba ya Jamhuri ya Kenya.

Sahihi
Mgombea Uchaguzi

Imeshuhudiwa na.....

(b) Wagombea Uchaguzi wa Urais na wa Ubunge:

1. Mwanachama wa Chama cha Kenya African National Union ambaye atataka kusimama kama mgombea uchaguzi wa Kiti cha Bunge sharti atume maombi kwenye fomu maalum ya maombi kama hayo kwa Rais wa Chama na aambatanishe maombi kama hayo na historia yake fupi kupitia kwa tawi lake. Nakala ya maombi hayo itumwe kwa Katibu Mkuu na iwe na maelezo yafuatayo:

- (i) Jina la mgombea uchaguzi.

(ii) Nambari yake iliyoandikishwa ya upigaji kura.

(iii) Namba yake ya uanachama.

(iv) Jina la tawi lake ndogo.

Ikiwa mwenye nia ya kugombea kiti—

(i) ana hati halisi ya uanachama wa maisha wa Chama;

(ii) hajatenda kosa lo lote la uhalifu au kuhusika na ufiisadi au vitendo vya uchochezi;

(iii) atatimiza masharti yote ya uchaguzi kulingana na katiba ya Kenya;

(iv) atajiuzulu madaraka yake Serikalini, Serikali za Wilaya, Halmashauri za Serikali au katika halmashauri ambazo zinamilikiwa nusu na Serikali na nusu na makampuni mengine au madaraka yote yale yanayodhaminiwa na Chama, miezi sita au zaidi kuanzia tarehe ya uteuzi wa uchaguzi wa mchujo.

2. Afisa Mkuu wa Kitaifa wa Chama atatoa fomu rasmi za KANU za maombi ya kugombea uchaguzi kwa mwenye nia ya kugombea uchaguzi na pia fomu za kiapo cha uaminifu. Kila mmoja atakayetuma maombi ya kutaka kugombea uchaguzi, atahitajika kujaza fomu moja ya maombi kwa ukamilifu na kisha aitume kwa Rais wa Chama ikiwa imeambatanishwa na maelezo mafupi kuhusu maisha ya mwenye maombi, kupitia kwa tawi linalohusika hali kadhalika nakala nyingine itumwe kwa Katibu Mkuu wa Chama.

3. Maombi hayo yataandamana na ada ya shilingi elfu tatu (Sh. 3,000) ambazo hazitarudishwa.

4. Kamati Kuu ya Wilaya itawahoji wote wanaotaka kugombea viti vya ubunge katika wilaya zao na kisha kutuma taarifa kwa Makao Makuu ya Chama.

5. Kila mgombea uchaguzi wa Chama cha Kenya African National Union atakayepigania uchaguzi wa Kiti cha Bunge atatia sahihi kiapo kifuatacho cha uaminifu. Fomu hii, baada ya kutiwa sahihi na mwenye maombi, itaambatanishwa na dhamana kama ilivyotajwa katika aya ya tatu katika kanuni hii.

Mimi
ningependa kuteuliwa na Chama cha Kenya African National Union kama mgombea uchaguzi katika uchaguzi ujao wa Kiti cha Bunge cha sehemu ya uchaguzi ya ,
na nina apa kwamba ikiwa nitachaguliwa kuwa mbunge, na wakati wote nitakuwa mbunge kwa niaba ya Chama cha Kenya African National Union—

- (a) nitaendelea kuwa mwaminifu kwa Rais na Chama;
- (b) nitaunga mkono kwa dhati katiba na mwongozo wa Chama na misingi yote ya Chama cha kukuza umoja miongoni mwa wananchi;
- (c) nitaunga mkono maongozi yote ya Serikali ya KANU; na
- (d) nitazingatia Katiba ya Jamhuri ya Kenya katika utekelezaji wa shughuli zangu zote.

Na nina jichukulia jukumu la kutekeleza na kuonyesha wazi wazi kiapo hiki changu hadharani katika sehemu yangu ya uchaguzi.

Tarehe ya siku ya , 19.....

Sahihi
Mgombea Uchaguzi

Shahidi

(c) Utaratibu wa kupiga kura na kutangaza matokeo:

1. (i) Utaratibu wa kupiga kura utakuwa kupiga mstari nyuma ya mgombea uchaguzi au maajenti wake halisi wawili, mmoja atakayebeba picha kubwa ya mgombea uchaguzi. Kura zitaaza

kupigwa saa sita mchana kote katika Jamhuri. Katika sehemu zingine lokesheni ndogo/wodi zitakuwa ni mahali tosha pa kupigia kura lakini shughuli hizo zitafanyiwa mahali na katika vituo ambavyo vitaandikishwa rasmi katika gazeti rasmi la serikali kuwa kama vituo vya upigaji kura, kama itakavyoamuriwa na msimamizi wa uchaguzi.

(ii) Wapigaji kura watabeba kadi halisi za uanachama wa KANU, kadi ya kupiga kura na kitambulisho cha kitaifa. Ikiwa kutatokea hali ya kutoamini Msimamizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kuchunguza tafdhali ya KANU.

2. Kura zitahesabiwa na Msimamizi wa Uchaguzi mbele ya maajenti halisi wa mgombea uchaguzi. Baada ya kuhesabu kura zote, idadi ya kura alizopata mgombea uchaguzi zitaandikwa kwenye stakabadhi maalum ambayo itatiwa sahihi na Msimamizi wa Uchaguzi na hali kadhalika mmoja wa maajenti wake halisi na nakala zote za stakabadhi hizi kufungiwa ndani ya bahasha. Kukitokea hali ambapo ajenti wa mmoja wa wagombea uchaguzi atakataa kutiwa sahihi stakabadhi hiyo, matukio hayo yaandikwe kwenye stakabadhi ya matokeo pia.

3. Baada ya uchaguzi kumalizika, matokeo yatapelekwa katika Makao Makuu ya Wilaya na Wasimamizi wa Uchaguzi ambapo watayatoa kwa Afisa Mkuu wa Uchaguzi katika Wilaya mbele ya maajenti wa wagombea uchaguzi kutoka vituo mbali mbali vya kupigia kura.

4. Mgombea kiti ambaye alishiriki kwenye uchaguzi na:

(a) Kupata asilimia 30 au zaidi ya kura zote zilizopigwa kwa jumla, atabaki kwenye pambano hilo.

(b) Kupata zaidi ya asilimia 70 ya jumla ya kura zilizopigwa atakuwa amerudishwa bila kupingwa katika uteuzi wa kiti cha Bunge/Serikali za Wilaya.

(c) Kwenye hali ambapo hakuna hata mmoja wa wagombea uchaguzi aliyewahi kupata asilimia 30 au zaidi ya kura zilizopigwa, basi wagombea uchaguzi wawili wa kwanza watateuliwa.

(d) Katika hali ambapo mmoja wa wagombea uchaguzi atapata asilimia 30 au zaidi ya jumla ya kura lakini akakosa kufikia kiwango cha juu zaidi na wengine wote wakapata chini ya asilimia 30 basi wagombea uchaguzi wawili wa kwanza wenye kura chini ya asilimia 30 watateuliwa kujiunga na yule aliyepata kura zaidi ya asilimia 30.

5. Tawi likisha pokea matokeo ya uchaguzi wa mchujo kutoka kwa Afisa Mkuu wa Uchaguzi katika Wilaya (Mkuu wa Wilaya), litatuma matokeo hayo moja kwa moja hadi Makao Makuu ya Chama ambapo orodha kamili ya wagombea uchaguzi wa Kanu itatayarishwa kwa Jamhuri nzima.

23. WADHAMINI

(a) Ardhi yote, majengo na mali yote mali ya Chama yataandikishwa katika majina ya wadhamini watano ambao watachaguliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Wajumbe wa Chama.

(b) Wadhamini watateuliwa na kutumika kwa muda wa miaka minne wala hawawezi kuondolewa afisini isipokuwa kwa sababu hizi zifuatazo—

(i) kujiuzulu kwao kwa hiari katika maandishi;

(ii) kufilisika kwa mdhamini; au

(iii) mdhamini afanye vitendo vibaya ambavyo vitalazimu kura kupigwa kumwondoa afisini. Baraza Kuu la Kitaifa kwa wingi wa kura wa theluthi mbili, ndilo litakalokuwa na uwezo wa kumwondoa afisini mdhamini kama huyo.

(c) Idadi ya kutosha ya kuuwezesha mkutano wa wadhamini ifanywe itakuwa wadhamini watatu.

(d) Wadhamini wanaweza kushtaki au kushtakiwa kwa mujibu wa mamlaka yao kama wadhamini wa Chama.

(e) Wadhamini watakusanya, kurekebisha na kukodisha mali ya Chama na kutoa taarifa yao ya kila mwaka kuhusu hesabu yao

ya fedha kwa Kamati Kuu ya Kitaifa ya Chama chini ya Sheria ya Udhhamini.

(f) Wadhamini watakuwa na uwezo wa kuuza, kununua na/au kubadilisha umilkaji wa rasilimali zo zote za Chama na kuzichumisha pesa zitakazopatikana katika hati za dhamana, mikopo ya nyumba, hisa, pamoja na aina nyinginezo za uchumishaji wa rasilmali kama itakavyoidhinishwa kwa maandishi na Kamati Kuu ya Kitaifa ya Chama cha Kanu.

(g) Wadhamini watalipa mapato yatakayopolewa kutoka kwa rasilmali iliyochoreshwa kwa Mweka Hazina Mkuu wa Kitaifa.

(h) Matawi yatateua wadhamini wasiozidi watatu katika mikutano yao Mikuu ya Kila Mwaka na wadhamini hao watazingatia masharti kama yale yanayowahusu wajumbe wanaohudhuria Mikutano ya Kitaifa ya Chama.

(i) Wadhamini watahitajika kuchaguliwa tena muda wao utakapomalizika.

24. NIDHAMU

(a) KOMITI YA KITAIFA YA NIDHAMU

(i) Komiti ya Kitaifa ya Nidhamu itakuwa na wanachama kumi na wanane walioteuliwa na Rais kama ifuatavyo:

—Wanachama tisa kushugulikia maswala ya mikoa, na

—Wanachama tisa kushugulikia maswala mengine.

(ii) Kutakuwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na Naibu wa Mwenyekiti atakayechaguliwa kutoka miongoni mwa wanakomiti wa nidhamu kwenye mkutano wake wa kwanza.

(iii) Afisa Mkuu wa Kitaifa wa Kenya African National Union atakuwa Katibu wa Komiti ya Nidhamu ya Kitaifa.

(iv) Komiti ya Nidhamu itakuwa na uwezo wa kusikiza na kuchunguza maswala yaliyopendekezwa na Komiti Kuu ya Tawi pamoja na maswala mengine yatakayoletwa mbele yake na Rais wa KANU, Komiti Kuu ya Kitaifa na Baraza Kuu la Kitaifa.

(v) Komiti ya Nidhamu itakuwa na utaratibu, kanuni na sheria za kuzingatwa zitakazoidhinishwa na Komiti Kuu ya Kitaifa na Baraza Kuu wakati wa kuendesha shughuli zake.

(b) Rais wa Chama atakuwa na uwezo wa kumsimamisha mwanachama ye yote ama afisa wa Chama kwa ukosefu wa nidhamu ama kutozingatia kanuni za katiba na kusimamishwa huko kutaendelea hadi Baraza Kuu la Kitaifa litakapoamua kuubatilisha ama kuuidhinisha.

(c) Kila komiti ya tawi itakuwa na uwezo wa kumsimamisha mwanachama ye yote afisa wa Chama katika wilaya. Hatua hiyo itaripotiwa kwa Komiti ya Nidhamu ya Kitaifa ambayo itachunguza na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu, kupitia kwa Komiti Kuu ya Kitaifa ambayo itakubali ama kukataa hatua ya kusimamishwa.

(d) Rais anaweza, kwa kushauriana na Komiti Kuu, kuteua tume itakayochunguza shughuli ama mienendo ya tawi lo lote, tawi ndogo katika lokesheni, lokesheni ndogo ama komiti ya wodi. Rais anaweza kuchukua hatua kuambatana na uamuzi uliofikiwa na tume, na uamuzi kama huo utaendelea kutumika hadi wakati Baraza Kuu la Kitaifa litakapoamua kuukataa ama kukubaliana nao.

(e) Rais anaweza, kwa kushauriana na Komiti Kuu, kuvunjilia mbali tawi lo lote ama Kundi la Chama na kuagiza uchaguzi mwingine ufanywe.

25. KUVUNJWA

Chama kinaweza, kwa azimio litakalopitishwa na sehemu ya theluthi 2/3 ya wanachama wengi kwenye Mkutano Maalum wa Wajumbe ulioitishwa kwa madhumuni ya kuvunjwa, kuazimia kwamba kitavunjwa. Iwapo kitavunjwa, mali yote na pesa za

Chama, baada ya mkutano, raslimali zote zitagawanywa kuambata na utaratibu utakaoamuliwa kwenye mkutano ambapo azimio la kutaka kuvunjwa litapitishwa.

26. KUELEWA MAANA

Kwenye katiba hii, iwapo haikuelezwa kwa njia inayostahili kueleweka:

(a) "Chama" ni kumaanisha Kenya African National Union (KANU).

(b) "Komiti ya Lokesheni/Wodi" ina maana ya kwamba ni komiti iliyochaguliwa na wanachama kuambatana na sehemu ya utawala ya lokesheni ama wodi.

(c) "Tawi Ndogo" ina maana ya sehemu ya uchaguzi inayowakilishwa katika Bunge la Taifa.

(d) "Komiti Kuu ya Tawi" ina maana ya komiti ya KANU iliyoko katika eneo la utawala la wilaya ikiwa ndiyo sehemu yenye tawi kama hilo.

“UHURU NA KAZI”

KANU YA JENGA NCHI